## MRADI WA KUBORESHA MAZINGIRA YA BIASHARA (LOCAL INVESTMENT CLIMATE)

### a) Dira ya Mradi;

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) kwa kushirikiana na Serikali ya Denmark kupitia Shirika la Maendeleo la DANIDA (Danish Development Agency) wanatekeleza Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (Local Investment Climate) kwa Njia ya Majadiliano ili kuwainua Wananchi Kiuchumi.

Mradi huu wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji unatekelezwa ili kukabiliana na changamoto za kibiashara ili kukabiliana na changamoto za kibiashara na Uwekezaji hususani zinazokwamisha kukua kwa biashara na maendeleo ya kiuchumi katika ngazi ya chini. Mradi umelenga kusaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na wananchi wanaojishughulisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi Vijijini na Mijini.

Mradi unahamasisha uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji kwa vitendo ili kutatua changamoto za kibiashara ambazo Serikali inakabiliana nazo katika kukuza uchumi, kuleta maendeleo, kukuza ajira na kuondoa umasikini katika Taifa letu. Mradi huu umeanzisha ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji katika Mikoa ya Kigoma na Dodoma ili kuchochea ukuaji wa kiuchumi, shughuli za biashara na uwekezajizinazofanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinaakisi na kutafsiri Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Maendeleo Endelevu ya Kimkakati (SDGs), Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 na mikakati mbalimbali ya Serikali.

Utekelezaji wa mradi pia unazingatia utekelezaji wa mkakati wa Serikali wa kuboresha mazingira ya biashara kwa baadhi ya maeneo yaliyoainishwa kwenye mkakati huo.

Mradi unaimarisha ushirikiano baina ya Serikali na Sekta binafisi katika kuboresha na kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuhakikisha upatikanaji wa ardhi, miundombinu ya msingi na huduma bora pamoja na majukwaa ya majadiliano.

**b) Lengo la Mradi;**

Mradi unalenga kuboresha mazingira ya biashara ili kuvutia uwekezaji na ukuaji wa biashara ya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopo katika Mikoa ya Dodoma na Kigoma ili kukuza uchumi, kuongeza ajira, kukuza vipato vya wananchi na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ujumla. Wanafaika wa mradi ni vikundi vya kijamii vinavyojishughulisha na shughuli za kiuchumi, jamii ya wafanyabiashara/wakulima/wafugaji na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**c) Wadau;**

Katika kuhakikisha kuwa mradi huu unatekelezwa kikamilifu, wadau mbalimbali wameshirikishwa ambao ni; Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa, Ofisi ya Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Jumuiya ya Tawala za MitaaTanzania (ALAT), Chemba ya Wafanyabiashara, Wakulima na Wenye Viwanda Tanzania (TCCIA) na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF).

**d) Utekelezaji wa mradi;**

i. Majadiliano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kupitia Mabaza ya Biashara katika ngazi ya Mikoa na Wilaya (District Bussiness Councils/Regional Bussiness Councils) yanayofanyika katika Mikoa ya Dodoma na Kigoma.

ii. Ujenzi na uendeshaji wa vituo vya kutolea huduma za biashara OSBC).

iii. Miradi ya ujenzi/uboreshaji wa miundombinu katika maeneo ya biashara, uwekezaji na kilimo pamoja na kuanzisha kongano kwa kuzingatia mnyororo wa thamani.

iv. Kuboresha miundombinu ya ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinabuni vyanzo vipya ili kuongeza wigo wa mapato, upimaji na uthaminishaji wa ardhi.

**e) Mafanikio ya mradi hadi kufikia Desemba, 2018;**

a) Kuanzishwa na kuendelezwa kwa Mabaraza ya Biashara ya Wilaya zote za Dodoma na Kigoma.

- Kuimarika kwa mahusiano na ushirikiano kati ya Sekta binafsi na Serikali.
- Kusainiwa na kuanza kutekelezwa kwa makubaliano ya pamoja kati ya sekta binafsi na Mamlaka za Serikali za Mitaa kushughulikia changamoto za kibiashara mkoani Kigoma.
- Kusainiwa makubaliano ya kushirikiana kati ya mabaraza ya biashara na Mabaraza ya Madiwani mkoani Dodoma.

- Mabadiliko ya sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikisha Sekta binafsi kama vile Mpwapwa, Chamwino na Bahi mkoani Dodoma.

b) Kuibuliwa na kuanza kutekelezwa kwa miaka 47 ya uwekezaji kama; (Uboreshwaji wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji, miundombinu ya masoko, minadi, machinjio, utafiti wa vyanzo vya maji, viwanda vidogo, upimaji wa ardhi) yenye thamani ya zaidi ya Tsh. 6.2 Bilioni yenye wanufaika wapatao 18,896 ambapo wanawake ni 6,586 na wanaume ni 12,310.

c) Mradi umewajengea uwezo wafugaji na wakulima wapatao 1,500 kwa kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali, kuwaandikia maandiko ya miradi na kuwaunganisha na Taasisi za fedha kwa ajili ya kupata mikopo ili kukuza mahitaji yao.

d) Kuanzishwa kwa vituo 13 vya utoaji wa huduma za biashara katika Halmashauri zote za mkoa wa Dodoma na Kigoma (One stop Centres) ambavyo vimepunguza urasimu wa utoaji wa huduma za biashara na kuongeza idadi ya biashara zinazosajiliwa na hivyo kuchangia mapato ya Halmashauri.

e) Mradi umekarabatikituo cha kutoa mafunzo ya kilimo na ufugaji kibiashara kwa nadharia na vitendo kwa vijana na wanawake kilichopo katika Halmshauri ya Wilaya ya Mpwapwa (Kibakwe Resource Centre). Mpaka sasa mafunzo yametolewa kwa vijana na wanawake wapatao 250.

f) Mradi unakamilisha ukarabati wa miundombinu, uandaaji wa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi, upimaji na utoaji wa Hati

za kimila katika miradi mikubwa ya uzalishaji kupitia kilimo cha umwagiliaji na makazi iliyopo katika Halmashauri za Kasulu, Bahi, Kondoa, Uvinza na Chamwino ambayo itawanufaisha zaidi ya wakulima na wafanyabiashara 9,266.

**f) Ubunifu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na ukusanyaji wa mapato kielekitroniki**

Katika eneo la kuboresha miundombinu ya ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha kuwa Halmashauri zinabuni vyanzo vipya ili kuongeza wigo wa mapato, mradi unatekeleza mambo yafuatayo:

- ❖ Mradi umeziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kununua mashine za kielektroniki za kukusanyia mapato (POS) 505 kwa ajili ya Halmashauri zote za Mikoa ya Dodoma na Kigoma.
- ❖ Mradi umewekeza zaidi ya Tsh. 2Bilioni kwa ajili ya manunuzi ya POS 235 za awali, kufunga mifumo ya kielektronikiya ukusanyaji mapato katika Halmashauri za Mikoa ya Dodoma na Kigoma ambao umeongeza makusanyo kwa asilimia 88 katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba, 2018 kwa Mikoa ya Dodoma na Kigoma na 130% kwa mkoa wa Dodoma katika kipindi husika.
- ❖ Mradi umeiwezesha OR-TAMISEMI kukamilisha maandalizi ya Mwongozo wa ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka za

Serikali za Mitaa (Revenue Management Guide) utakaozisaidia Halmashauri.

**g) Matarajio ya mradi;**

Mradi unatarajia kuleta mageuzi ya kiuchumi kwa vitendo na kubadilisha hali ya uchumi wa jamii, kupunguza gharama na vikwazo vya kibiashara huku ukiimarisha Sekta Binafsi ili iweze kukabiliana na ushindani na kuwa msingi thabiti wa mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Matarajio ya mradi ifikapo mwaka 2020 ni yafuatayo:

1. Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopo kwenye mradi kutumia majukwaa ya majadiliano kama fursa muhimu katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.
2. Jamii ya wafanyabiashara/wakulima/ wafugaji kuwa na sauti moja, kupata taarifa za biashara na kutumia fursa hiyo kuanzisha na kuendeleza biashara.
3. Sekta ya Umma/Serikali na Sekta Binafsi kushirikiana katika kuendeleza midahalo ya kibiashara ili kukabiliana na changamoto na kuondoa vikwazo vya kibiashara na uwekezaji vilivyopo katika maeneo yao.

Uzoefu utakaopatikana kupitia utekelezaji wa Mradi huu wa Kuboresha Mazingira ya Biashara utatumika kuandaa mifumo mbalimbali (models) itakayotumiwa na Halmashauri Tanzania Bara. Kwa taarifa zaidi tembelea tovuti ya mradi kwa anuani ya barua pepe ya https://www.lic.or.tz/p/about-us